

HALAMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA
MTIHANI WA PILI WA KUJISOMEA NYUMBANI
DARASA LA NNE 2020

SOMO: KISWAHILI

JINA: _____ **SHULE:** _____

MUDA: SAA 1:30 _____ **JUNI, 2020**

MAELEKEZO

- i. Mtihani una jumla ya maswali matano (5)
- ii. Jibu maswali yote kwa usahihi .

SEHEMU A: IMLA

1. Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa na msimamizi wa mtihani kisha uziandike kwa usahihi.

- i. _____
- ii. _____
- iii. _____
- iv. _____
- v. _____

SEHEMU B: SARUFI NA MISAMIATI

2. Chagua herufi ya jibu sahihi kisha uandike jibu katika kisanduku.

- i. _____ Mwalimu alifundisha somo la kiswahili.
a) Jana b) Leo c) Kesho d) Keshokutwa ()
- ii. Mtu asiyesikia ni _____
a) Kipofu b) Kibogoyo c) Kiziwi d) bubu ()
- iii. Mbuni ni _____

a) ndege mkubwa b) mmea mdogo c) nyoka mrefu d) samaki ()

iv. Kiranja ni kiongozi wa _____

a) walimu b) wazazi c) watu d) wanafunzi ()

v. Fundi _____ hushona suruali na magauni

a) mwashi b) cherehani c) viatu d) seremala ()

SEHEMU C: MATUMIZI YA LUGHA

3. Jibu maswali haya kutokana na ulivyouliozwa.

i. Ridhika na kila ulichokipata kwa sababu _____ huinukia koroma.

(mchagua sana, mtembea sana, mtafuata sana)

ii. Walimu walimpa adhabu kwa sababu alionekana ana _____.

(kibali, kiburi, kibuli)

iii. Askari _____ cha utii kwa Rais.

(walikula usia, walikula kiapo, walikula ahadi)

iv. Kiota changu nimekizungushia boma la nyasi _____.(kisogo, zizi, macho)

v. Hana miguu lakini huenda mbio sana _____.(nyoka, konokono, mnyoo)

SEHEMU D: UTUNGAJI

4. Tumia maneno yafuatayo kukamilisha insha hii.

wanyama, maisha, salama, jangwani, viumbe.

Maji ni muhimu kwa (1)_____ya viumbe hai. Mahali pasipo na maji (2) _____ hai haviwezi kuishi. (3)_____ hakuna maji ya kutosha. Maji kidogo yaliyopo hayatoshi kwa mahitaji ya watu na (4) _____.

Binadamu ana matumizi mengi ya maji. Anahitaji maji kwa ajili ya kufulia, kuogea na kusafishia vyombo. Pia anahitaji maji kwa ajili ya kunywa na kupikia. Maji ya kunywa lazima yawe safi na (5) _____.

SEHEMU E: UFAHAMU

5. Panga sentensi zifuatazo kwa kuandika namba 1 hadi 5 kwenye mabano ili zilete mtiririko mzuri wa maana

1. Shule ni mahali pazuri ()
2. Maarifa wanayopata ni akiba yao ya baadae ()
3. Wale ambao watayatumia vizuri yatawawezesha kuishi kwa kujitegemea ()
4. Watayatumia wakiwa bado shuleni au baadaye wakiwa wakubwa ()
5. Wanafunzi hujifunza maarifa mengi ()

IMLA

1. Sisi tunakula nyama ya ng'ombe
2. Mbwa anakula majani
3. Tunafua nguo zetu za nyumbani
4. Walipofika nyumbani kwetu walifurahia mazingira
5. Watoto wanacheza ngoma